

MATUMAINI PROG NO:2528

TITLE: HOW LONG HALT YE BETWEEN TWO OPINIONS?

SUMMERY: KINAZUNGUMZIA KUHUSU KUTUAFUTA SULUHISHO LA JAMBO
KUPITIA KWA MUNGU KWANZA.

TEXT: 1 WAFALME 18:17-40

MADA: UTASITA-SITA HADI LINI?

.....

Natuome kwanza kabla ya kusonga mbele;
OMBI.... Jehovah Rafa,,Jehovah Shammah, Jehovah Nissi; tunakushukuru kwa
ulinzi na zaidi mno uwepo wako katika anga hizi kupitia kwa kipindi hiki.
Tunapozama kwenye somo hili la leo, fungua mioyo yetu tulielewe vyema.
Katika jina la Yesu, Amina.

Mtu wangu, ni wakati mwingine wa kufurahi kwa kuwa Mungu wetu
Ametukutanisha tena ili tukajifunze kutoka katika Neno lake. Ni tumaini langu
kwamba unaendelea vyema.
Karibu ili tukalianze somo letu la leo lenye kichwa ambacho ni swali ya
kwamba,,,*utasita-sita hadi lini?*

Hiki ni kipindi cha Matumaini kutoka TWR Kenya.
Somo ni kutoka kwenye 1 Wafalme 18:17-40.

Kwa kumalizia fundisho hili,, nitakuwa na kupatia anwani yangu ya mawasiliano
kati yangu nawe.

Nataka kwanza kabisa ukabarikiwe kupitia kwa wimbo ambao unasema ya
kwamba,, nimekuachia wewe

WIMBO:

Ni wana-Christ Followers na wimbo Nimekuwachia wewe..Asanteni sana
watumishi wetu na Mungu Awabariki sana.....
Mimi naitwa, Vincent Amara.

Mpendwa unayeniskiza,,sisi kama wanadamu,,jambo la kujiamulia mambo bila
shaka ni sehemu ambayo ni ya lazima kabisa ya utu na nafsi yetu.Sisi

hatukuwekewa programu maalum kama vile ya mashine, na wala hatuishi kwa silika au (instincts) tu kama wanyama.

Rafiki yangu,, sisi tunaishi kwa kutumia akili ambayo inatuelekeza katika kuyaafikia maamuzi yetu. Lakini ili kufanya maamuzi sahihi, ni lazima tuwe na ukweli kamili.

Kwa wakati mwingine,,, kwetu sisi huwa ni vigumu kuamua kati ya mambo mawili ambapo akili zetu husumbuka sana ili kuafikia suluhisho. Jambo hili bila shaka hutufunya kutetemeka kutoka ndani.

Hapa tunayo maswali mawili tena makuu zaidi.

Swali la kwanza ni,,, Je, tunayafanyaje maamuzi? Na la pili ni,,, mbona sisi husita-sita na kuyumba katika kuamua kati ya mambo mawili?

Tunapoyarejelea maandiko kwenye kitabu cha Agano la kale yaani 1 Wafalme 18:17-40,,, tunapata kouona ya kwamba,, Nabii Eliya na taifa la Israeli walikabiliwa na wakati kama huo katika historia,,, yaani kuchagua kati ya mambo mawili ili kuamua haraka.

Dadangu mpendwa,,, kutokana na fungu hili la neno,,, tunamwoona Nabii Eliya akiwa anawauliza swali hili kuu; yaani kwamba,, "Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini?"

Mpendwa,,, hili ndilo lilikuwa jaribio lao kuu. Nikiwa nazingatia aya za kimsingi pekee kutokana na fungu hili la neno,,,,,,, yaani kutoka kwenye kitabu cha 1 Wafalme 18:17-40,,, bila shaka tunaenda kuipata hadithi kuhusiana na uzoefu huo.

Ningependa kukushirikisha aya za 21,38,39, ambapo Biblia inasema hivi;

21. Eliya akawakaribia watu wote, akasema, "Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Kama Bwana ndiye Mungu, mfuateni; bali kama Baali ndiye, mfuateni yeye." Na hao watu hawakumjibu neno.

38. Ndipo moto wa Bwana ukashuka, ukateketeza sadaka ya kuteketezwa, na kuni, na mawe, na mavumbi, ukayaramba na yale maji yaliyokuwamo katika mfereji.

39. Na watu wote walipona, wakaanguka kifudifudi, wakasema, "Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu."

Ndugu pamoja na dadangu,,, ili kuelewa vizuri, Eliya alifuata hatua tatu kubwa ili kuwasaidia Waisraeli kufanya uamuzi sahihi.

Kipengele cha kwanza kabisa,,, ni pale ambapo tunamwoona Nabii wa Mnugu Eliya Akitoa Changamoto Kuu. Bwana alimwambia Eliya aende akajionyeshe kwa Mfalme Ahabu. Wakati huo hali ilikuwa mbaya sana nchini; mbingu zilikuwa zimefungwa na kukuwa hakuna mvua kwa miaka mitatu kutokana na uasi wa Mfalme Ahabu na mkewe Yezebeli, waliomleta mungu wa uongo,,kwa jina Baali na kuabudiwa na wan awa-Israeli.

Mfalme Ahabu alipomwona Eliya, Neno linatuambia kuwa,,,alimshutumu akisema, *"Je! Ni wewe, unayeisumbua Israeli?"* Lakini Eliya alimjibu kwa ujasiri na kumwambia kuwa mfalme na nyumba ya baba yake ndio walioleta taabu hiyo kwa kuziacha amri za Bwana na kumfuata Baali.

Rafiki yangu,,,Eliya alisimama katika nafasi yenye ushawishi mkubwa, akaitisha mkutano wa taifa zima pale Mlima Karmeli pamoja na manabii 450 wa Baali. Akatoa changamoto kwao na kuwaamrisha hivi,,,Chagueni leo kati ya Baali na Mungu wa kweli.

Nabii huyu,, Alipendekeza wajenge madhabahu mawili na kuweka ng'ombe wawili bila ya kuwasha moto wao wenyewe.

Neno linituambia kwamba,,, walikubaliana kuwa Mungu atakayejibu kwa moto, huyo ndiye atakayeitwa Mungu wa kweli!. Waliokuwa wakisikiliza,,, wote tunaambiwa walitikia na kusema , *"Umesema vema!"*

Mpendwa,,huenda leo uko katika hali ya kushindwa kuchagua kati ya mambo mawili,, na unayumba katikati ya mawazo mawili. Nakuhimiza hivi,,wewe mtafute Mwenyezi Mungu, maana uamuzi wako ndio utakao kuamulia hatma yako ya kesho!

Kipengele cha pili,,tunamshuhudia,,, Nabii Eliya akiwa analisimamia shindano hilo. Kutokana na fungu hili la neno,,,tunaambiwa kuwa,,,aliwaambia manabii wa Baali watangulie maana wao ndio walikuwa wengi. Walimtayarisha ng'ombe wao, wakamweka juu ya madhabahu, na kuanza kuomba. Swali ni,,,manabii hao waliomba nini?

Bibilia inatuambia kuwa ni maneno manne tu yaliyorudiwa rudiwa kwa kukata tamaa: Yaani,, "Ee Baali, utusikie! Ee Baali, utusikie!" Wakawa wanaruka-ruka juu ya madhabahu wakifanya Ishara nying ili sanamu huyo akaweze kuwaskia.

Bibilia ina tuambia,,,,Eliya alianza kuwadhihaki akisema: "Pigeni kelele sana, kwa kuwa yeye ni mungu; labda anafikiri, au amekwenda kando, au yuko safarini, au labda amelala, yafaa aamshwe!"

Tunaambiwa,,walipiga kelele zaidi, wakajikata-kata kwa visu na mishale hadi damu ikawatoka. Lakini neno linasema: "Hapakuwa na sauti, wala aliyejibu, wala aliyejali." Kelele zao ziliishia kuwa za bure tu maana hakuna kilichotokea.

Kisha, Eliya akawaita watu wote wamkaribie, akaitengeneza madhabahu ya Bwana iliyokuwa imebomoka na kutelekezwa kwa muda mrefu. Alichagua mawe kumi na mbili kulingana na kabila za Israeli, akajenga madhabahu kwa jina la Bwana, akachimba mfereji mkubwa pembeni, akaweka kuni, na kumkata yule ng'ombe vipande vipande.

Ili kuondoa shaka yoyote ya udanganyifu, aliamuru madhabahu na sadaka imwagiwe mapipa manne ya maji mara tatu mfululizo, hadi maji yakajaa kwenye mfereji! Kila kitu kilikuwa tayari kwa ajili ya kumalizia.

Kipengele cha tatu na cha mwisho kwa leo kutokana na fungu hili ni,,,,, Eliya alishinda kwa kumalizia au mwishowe. Eliya alikaribia na kuomba maombi mafupi, rahisi lakini yenye nguvu ya kiungu, tofauti na makelele ya wale manabii wa uongo.

Bibilia inasema,,,aliomba akisema: "Bwana, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo hii ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako... Usikie, Ee Bwana, usikie, watu hawa wajue ya kuwa wewe, Bwana, ndiwe Mungu."

Mpendwa,,, huyu ni alikuwa mtu mmoja tu dhidi ya manabii wa uongo 450 na umati mkubwa wa watu. Alisimama peke yake, lakini alipoomba maombi yale rahisi, Mungu alijibu!

Moto wa Bwana ulishuka kutoka mbinguni ukateketeza kila kitu yaani ,,sadaka, kuni, mawe, mavumbi, na kuyaramba maji yote yaliyokuwa kwenye mfereji!

Ushuhuda ulikuwa wazi kabisa kiasi kwamba watu wote walianguka kifudufudi na kupiga kelele wakisema, "Bwana ndiye Mungu! Bwana ndiye Mungu!"

Lakini haikuishia hapo ndugu yangu. Eliya aliamuru manabii wote wa Baali wakamatwe, asitoroke hata mmoja, akawashusha hadi kwenye kijito cha Kishoni na kuwaua wote huko ili kuisafisha nchi na ibada za uongo.

Eliya alishinda kwa kishindo kikubwa kwa sababu alikuwa upande wa Mungu. Kama wasemavyo: Mtu mmoja aliye upande wa Mungu ni wengi kuliko umati wote yaani kwa kiingereza, "One with God is a majority". Mungu alimheshimu na kuiletea nchi ile mvua kubwa ya kuburudisha baada ya ukame wa muda mrefu.

Ninalo swali kwako mpendwa wangu, Je!, unapokabiliwa na maamuzi magumu maishani mwako leo, unapaswa kufanya nini?

Naomba kulipata jibu lako kupitia kwa maelekezo nitakayo kupa hapo baadae.

Eliya ameweka jambo hili wazi kabisa kwako,,,kwamba,,,mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini?

Mpendwa,,,nakusihi hivi,,,wewe kibinafsi,,,angalia sana kwa makini unapofanya uamuzi wako, kuwa mtaratibu mbele za Mungu na kuacha nafasi ya mashaka, na mwishowe ishi maisha ya ushindi katika uamuzi huo.

Fanya uamuzi wako ukiwa upande wa Mungu. Kumbuka, ukiwa na Mungu,,bila shaka unakuwa mshindi maana Yeye huwa upande wako kila wakati.Mungu wetu ndiye ajibuye kwa moto!

Natumai ya kwamba umepata kitu kizuri kutokana na fundisho hili la leo.

Amina!

Ombi.....

Uliye tukuka Juu ya vyote na tena Mfalme wa wafalme,,tunakushukuru kwa ajili ya fundisho hili leo ambalo ni la kutia moyo zaidi. Kwa kweli tutalizingatia kupitia kwa usaidizi wa Roho wako Mtakatifu.

Ni kwa Yesu tumeomba.....Amen.....

Rafiki yangu,,hiki Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu. Kipindi cha matumaini kutoka Twr.Leo mada yetu imekuwa ni;Utasita-sita hadi lini?

Tumeutoa kwenye 1 Wafalme 18:17-40.

Nitakuomba uwasiliane nami kupitia kwa anwani nitakayo kusomea mwishoni mwa kipindiki hiki cha leo. Anwani hiyo ni kwa ajili ya kusaidiana nawe.

Kabla yake,,u hapa wimbo,, Mungu ni Mungu Tu.....

WIMBO.....

Na kwa kweli kabisa Mungu atasalia tu kuwa Mungu....Asante sana mtumishi

Chris mwahangila kwa wimbo huo mzuri.

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA

KUTUMA KWA:

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe-barua@twr.co.ke

Kwenye Youtube ni @twr.co.ke

Mungu na akubarki sana Msikilizaji popote ulipo na,, hadi wakati mwingine, jina langu ni Vincent Amara.....Kwaheri